
WCF
Workers Compensation Fund
ISO 9001: 2015 CERTIFIED

FIDIA

# eNewsletter

TOLEO LA TATU | JULAI-SEPTEMBA 2024




## YALIYOMO


> WCF Yawagusa wakulima nchini
> Waziri Mkuu Majaliwa aipa kongole WCF kwa huduma bora
> Maafisa kazi watakiwa kutoa taarifa za wafanyakazi wanaoumia kazini

# Fidia Mtandaoni



1. Usajili wa waajiri na hati ya usajili
2. Kuwasilisha taarifa ya mapato ya mwaka ya wafanyakazi
3. Kuwasilisha michango ya kila mwezi kupitia namba ya udhibiti na kupata stakabadhi
4. Kuwasilisha taarifa ya ajali, ugonjwa ama kifo kitokanacho na kazi
5. Kuhusisha taarifa za wafanyakazi na mwajiri
6. Kupata mrejesho madai ya fidia

---

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano kwa Umma WCF:





**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)**

Jengo la Kambarage,
Ghorofa ya 3,
S. L. P 329, 41104 Dodoma.



**TIMU YA WAHARIRI**

MWENYEKITI
**Dkt. John Mduma**

MHARIRI
**Laura Kunenge**

MHARIRI MSAIDIZI
**Mcharo Mrutu**

WACHANGIAJI
**Meseka Kadala**
**Sophia Mtakasimba**

# Ujumbe Kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu



**Dkt. John Mduma**
**Mkurugenzi Mkuu WCF**

## Mpendwa Msomaji,

Kwa mara nyingine ninayo furaha kubwa kuwakaribisha katika toleo la tatu la Jarida letu la Fidia ambalo huandaliwa kwa lengo la kuwapasha habari wadau wetu kuhusu kazi mbalimbali zilizotekelezwa na Mfuko katika kipindi cha robo mwaka husika. Toleo hili linajumuisha habari kuhusu kazi na matukio mbalimbali yaliyotekelezwa na Mfuko katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Septemba, 2024.

Jambo la muhimu zaidi ambalo ningependa kuwashirikisha ni juu ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kukabidhiwa cheti cha ithibati ya utoaji huduma bora kwa viwango vya kimataifa (ISO Certification). Hii ni hatua muhimu sana kwa WCF kwa kuwa inazidi kutujengea imani kwa wateja na wadau wetu juu ya huduma tunazowapatia. Tunajivunia hatua hii na tunaamini kwamba itasaidia kuongeza ufanisi wa huduma zetu na tunatoa ahadi kwa wadau wetu kuwa tutazidi kuboresha utoaji wa huduma zetu hasa katika kuimarisha matumizi ya mifumo ya Tehama.

Katika ulimwengu wa leo, ambapo habari na mawasiliano ni muhimu zaidi kuliko wakati mwingine wowote, jarida hili linatuwezesha kuwasiliana kwa uwazi na wateja wetu na kupata mrejesho kuhusu huduma zetu. Tunaamini kuwa huduma zetu zinaweza kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya wateja wetu na kila hatua tunayoichukua inaimarisha dhamira yetu ya kuwahudumia kwa njia bora zaidi.

Asanteni sana kwa kuendelea kuwa sehemu ya safari yetu. Tunathamini sana ushirikiano wenu na tunatarajia kwamba kwa pamoja tutaweza kufikia malengo makubwa zaidi. Tafadhali jisikie huru kuuliza maswali, kutoa maoni au ushauri kuhusu namna tunaweza kuboresha huduma zetu zaidi.

*Ahsanteni na niwatakie usomaji mwema!.*

# WCF Yawagusa Wakulima Nchini



*Mh. Rais akishuhudia mazoa yanayozalishwa na wakulima wadogo wadogo wa maeneo ya mashambani mjini Unguja, Zanzibar.*

## Na Mwandishi wetu

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umetoa miche ya miti na matunda kwa ajili ya kusaidia uhifadhi wa mazingira kupitia wakulima wadogo wadogo wa maeneo ya mashambani mjini Unguja, Zanzibar.

Msaada huo ulikabidhiwa mwezi Agosti, 2024 mjini Makunduchi Zanzibar kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ufungaji wa mafunzo kwa vikundi vya wakulima kutoka maeneo mbalimbali nchini ikiwa ni sehemu ya kazi mbalimbali zilizotekelezwa wakati wa tamasha la Kizmkazi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma, alisema msaada huo sio tu unakwenda kuwainua wananchi kiuchumi, lakini pia kusaidia juhudi za Serikali za kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

Akizungumza mara baada ya kukabidhiwa msaada huo kwa niaba ya wakulima hao, Mhe. Rais Dkt. Samia aliipongeza WCF kwa kutambua umuhimu na kuwawezesha wakulima kutoka maeneo mbalimbali nchini ambao bado ni tegemeo kubwa katika ukuaji wa Uchumi wa Taifa.

"WCF ni Taasisi ya hifadhi ya jamii, na jamii bora inahitaji mazingira bora na sisi tumeona katika kusaidia Serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi, tutoe mchango wetu kwa kununua miche ya miti na matunda, ili ikasaidie Zanzibar ya kijani," alisema Dkt. Mduma.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea mfano hundi kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. John Mduma kwa ajili ya kusaidia uhifadhi wa mazingira kupitia wakulima wadogo wadogo wa maeneo ya mashambani mjini Unguja, Zanzibar.*

# WCF yapongezwa kwa Ithibati ya ISO ya utoaji wa huduma kwa viwango vya Kimataifa




*Katibu Mkuu – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Bi. Mary Maganga akikabidhi Cheti cha ISO kwa Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma*

## Na Mwandishi wetu

Katibu Mkuu – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu bi. Mary Maganga ameuagiza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kuhakikisha inazingatia ubora wa huduma inazotoa kwa wananchi ili kuendana na ithibati ya utoaji wa huduma kwa viwango vya kimataifa, waliyopata.

Amesema hayo jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya WCF kukabidhiwa Cheti cha Ithibati ya utoaji wa huduma bora kwa viwango vya kimataifa (ISO certification).

Akikabidhi cheti hicho kwa Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma, Bi. Maganga alisisitiza kuwa maboresho yanayofanywa na Mfuko huo yanapaswa kuzingatia mahitaji na matarajio ya wateja wake ili kuhakikisha wafanyakazi wanapatiwa haki yao ya fidia stahiki pale wanapopatwa na madhila yatokanayo na kazi zao.

"Kitu cha msingi ni kuhakikisha mnaendelea kuboresha mifumo ya utoaji wa huduma zenu. Nasisitiza mtumie ithibati hii mliyoipata kurahisisha taratibu za kuwasajili waajiri ili ikiwezekana waweze kujisajili wenyewe kwa hiari badala ya kulazimishwa kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria," amesema Bi. Maganga.

"Tumewekeza katika matumizi ya Tehama, ambapo kwa sasa takribani asilimia tisini ya huduma za Mfuko zinapatikana kwa njia ya mtandao ikiwemo usajili, kutoa taarifa ya madhila kutokana na kazi na kurekebisha taarifa za wafanyakazi. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaoishi maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, aliyeelekeza kwamba mifumo ya taasisi zote ni vyema isomane ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi," amesema Dkt. Mduma.




*Katibu Mkuu – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Bi. Mary Maganga akipokea Cheti cha ISO kutoka kwa mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Bi. Viola Masako.*

Aidha, Katibu Mkuu huyo ameongeza kuwa jitihada za kutoa elimu kwa wadau wake pamoja na kutumia matokeo ya tafiti mbalimbali ili kuhakikisha huduma zake zinakidhi mahitaji ya wateja ni muhimu kuzingatiwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma amebainisha kuwa mafanikio waliyoyapata yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji mkubwa wanaofanya katika matumizi ya mifumo ya Tehama. Ametoa rai kwa wadau wa Mfuko huo kutumia huduma za mtandao katika kupata huduma mbalimbali zitolewazo na WCF.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Bi. Viola Masako ameipongeza WCF kwa juhudi kubwa za utendaji hadi kufikia mafanikio hayo yanayoonesha nia thabiti ya Mfuko kuwajibika katika utoaji wa huduma kwa wateja wake kwa viwango vya kimataifa.




*Katibu Mkuu Bi. Mary Maganga akiwa kwenye picha ya pamoja na wageni mbalimbali waliohudhuria hafla hiyo*

"TBS tunaipongeza WCF na tumeshukuru kwa jambo hili kwa sababu linatuongezea wigo wa kuisaidia Serikali yetu kutekeleza majukumu yake kwa wakati na pia kujipima namna ya kuboresha zaidi utoaji wa huduma zake kwa wananchi," amesema Bi. Masako.

WCF ni Taasisi ya Hifadhi ya Jamii iliyochini ya Ofisi ya Waziri Mkuu yenye jukumu la kutoa fidia kwa wafanyakazi pale wanapoumia, kuugua kutokana na kazi wanazozifanya kwa mujibu wa mikataba ya ajira zao na pale mfanyakazi anapofariki kutokana na kazi wategemezi wa familia yake

# Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar apongeza ushirikiano wa WCF na ZSSF

**Na Mwandishi wetu**

Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdullah, amepongeza ushirikiano katika utendaji kazi baina ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF).

Mhe. Abdullah amesema hayo mara baada ya kushuhudia utiaji saini mkataba wa mashirikiano (MoU) baina ya taasisi hizo katika nyanja mbalimbali za utekelezaji wa majukumu yao, hafla iliyofanyika mwezi Julai, 2024 mjini Unguja sambamba na ufunguzi wa kikao kazi baina ya WCF na watendaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania pamoja na Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Mhe. Abdullah amesema mashirikiano hayo ni hatua mojawapo ya kutekeleza kwa vitendo azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuzitaka taasisi zisizo za muungano kutekeleza majukumu yao kwa kushirikiana.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi – WCF, Dkt. John Mduma (kulia) na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar - ZSSF Bw. Nassor Ameir (kushoto) wakionesha nyaraka mara baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano katika utendaji kazi*

"Nitoe wito kwa taasisi nyingine kuiga mfano huu ambao unachangia kujenga mahusiano mema lakini pia kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku," alisema Mhe. Abdullah na kuongeza kuwa "sote tumeshuhudia hatua ya utiaji saini ya mashirikiano baina ya WCF na ZSSF hivyo ni wazi kuwa mifuko hii sasa itazidisha ukaribu baina yao ambao utasaidia zaidi katika kupeana uzoefu na kutatua changamoto zitakazoibuliwa katika kutoa Mafao ya wafanyakazi wanaoumia au kupata ugonjwa unaotokana na kazi zao."



*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi -WCF, Dkt. John Mduma (kulia) na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar – ZSSF, Bw. Nassor Shaaban Ameir (kushoto) wakibadilishana nyaraka mara baada ya kusaini makubaliano ya ushirikiano katika utendaji kazi.*

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Bi. Mary Maganga, alisema usimamizi wa masuala ya hifadhi ya jamii yapo chini ya Ofisi yake na kupongeza hatua hiyo ya kurasimisha mashirikiano baina ya WCF na ZSSF ambayo huenda ikaongeza tija na ufanisi katika mchakato wa utoaji wa fidia kwa wafanyakazi wanaopata madhila yanayotokana na kazi zao katika pande zote mbili za Muungano.

Mkataba wa mashirikiano katika utendaji kazi baina ya taasisi hizo umesainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma na Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZSSF, Bw. Nassor Shaaban Ameir.

Hafla hiyo ilienda sambamba na ufunguzi wa kikao kazi baina ya WCF na watendaji wa Divisheni za Mahakama Kuu ya Tanzania pamoja na Mahakama Kuu ya Zanzibar ambayo ilihudhuriwa na Jaji Kiongozi, Mhe. Mustapher Siyani, (ambaye alimuwakilisha Jaji Mkuu wa Tanzania, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Khamis Ramadhan Abdallah, Majaji wa Mahakama Kuu Tanzania na wa Mahakama Kuu ya Zanzibar.

"WCF ni Taasisi ya hifadhi ya jamii, na jamii bora inahitaji mazingira bora na sisi tumeona katika kusaidia Serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi, tutoe mchango wetu kwa kununua miche ya miti na matunda, ili ikasaidie Zanzibar ya kijani," alisema Dkt. Mduma.



*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. John Mduma akibamkabidhi Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Hemed Suleiman Abdullah vitendea kazi wakati alipomtembelea Ofisini Kwake mjini Unguja.*

# Waziri Mkuu Majaliwa aipa kongole WCF kwa huduma bora




*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Meneja Tathmini ya Vihatarishi Mahala pa Kazi wa WCF Bi. Naanjela Msangi kuhusu kazi zinazotekelezwa na Mfuko katika kuwahudumia wafanyakazi wanaoumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi zao.*

## Na Mwandishi wetu

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, amesifu kazi nzuri inayofanywa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) katika kuwahudumia wafanyakazi wanaoumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi.

Mhe. Majaliwa alitoa pongezi hizo mwezi Agosti, 2024 jijini Arusha alipotembelea banda la WCF wakati wa maonesho yaliyoambatana na kongamano la tatu la Madereva wa Serikali. Akiwa katika banda hilo Mhe. Majaliwa alielezewa na Meneja Tathmini ya Vihatarishi Mahala pa Kazi wa WCF Bi. Naanjela Msangi kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Mfuko katika kuwahudumia wafanyakazi wanaoumia, kuugua ama kufariki kutokana na kazi zao.

"Mnafanya kazi nzuri sana, endeleeni kutoa huduma bora na muwaelimishe hawa madereva wa serikali kuwa makini wanapotekeleza majukumu yao, lakini wanapopatwa na changamoto muwaeleze utaratibu wa kufuatwa ili waweze kupata huduma," alisisitiza Mhe. Majaliwa.

Aidha, Meneja Tathmini ya Vihatarishi Mahala pa Kazi, WCF Bi. Naanjela Msangi, alimueleza Waziri Mkuu Majaliwa kuwa, madereva wa serikali ni sehemu ya wafanyakazi wa Umma ambao WCF inawahudumia.

"Tuko hapa kutoa elimu kuhusu huduma za Mfuko ili wadau na washiriki wa kongamano hili waweze kujua stahiki zao endapo watapatwa na madhila yanayotokana na kazi zao pamoja na taratibu za kuwasilisha madai pindi wanapopatwa na madhila wanapotekeleza majukumu ya mwajiri. Lakini pia tunawapa elimu ya jinsi ya kuepuka ajali za barabarani," alifafanua Bi. Msangi.

# Maafisa kazi watakiwa kutoa Taarifa za wafanyakazi wanaoumia kazini




*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete akizungumza na maafisa kazi kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania bara*

## Na Mwandishi wetu

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete amewataka maafisa kazi kote nchini kushirikiana na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kutoa taarifa za wafanyakazi wanaoumia maeneo ya kazi kwa wakati ili waweze kupewa stahiki zao kama Sheria inavyotaka.

Mhe. Waziri Kikwete ametoa wito huo tarehe 30 Agosti, 2024 jijini Arusha wakati wa ufunguzi wa kikao kazi baina ya WCF na maafisa kazi kutoka mikoa ya Tanzania bara ambapo aliwataka maafisa kazi hao kusimamia sheria za kazi kwa kufanya kaguzi mahala pa kazi ili kuhakikisha waajiri wanatekeleza matakwa ya sheria ya fidia kwa wafanyakazi.

"Jukumu lenu maafisa kazi ni kusikiliza malalamiko na kwa shughuli zinazohusu WCF jukumu lenu ni kuandika na kutoa taarifa WCF, sio kugeuka washauri wa waajiri ili kudhulumu haki za wafanyakazi, " amesema na kuongeza: "andikeni vitu ambavyo mwisho wa siku wafanyakazi watapata haki zao na sio kuandika ili sheria ionekane haifai," amesema Waziri Kikwete.

Aidha, Mhe. Kikwete amewataka maafisa kazi hao kusoma na kuelewa vizuri muswada wa mabadiliko ya sheria ya huduma za jamii, 2024 ambayo inahusu pia mabadiliko katika Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi ili waweze kuwa wasimamizi wazuri wa sheria hiyo mara baada ya kuwekwa sahihi na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Munngano wa Tanzania.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma alisema kwamba Mfuko huo umejizatiti katika kuhakikisha huduma zake zinapatikana kupitia mtandao pamoja na kuimarisha ushirikiano na Idara ya Kazi kupitia maafisa kazi hao kwa lengo la kuhakikisha kiwango cha ukidhi (compliance) wa uzingatiaji wa sheria ya fidia kwa wafanyakazi kinaongezeka.

"Kwa sasa huduma zetu kwa zaidi ya asilimia 90 zinapatikana mtandaoni, lakini pia tumekuwa tukishirikiana vizuri na wenzetu wa Idara ya Kazi kupitia maafisa kazi hawa ambao kiukweli ushirikiano huu umesaidia 'compliance' kwa upande wetu," alisema Dkt. Mduma.

Naye Kamishna wa Kazi Bi. Suzan Mkangwa alisema Ofisi yake imekuwa ikishirikiana na WCF katika kuhakikisha malalamiko ya wafanyakazi wanaoumia au kupata ugonjwa unaotokana na kazi zao yanatatuliwa kwa wakati.

Maafisa kazi 78 kutoka mikoa yote ya Tanzania bara wamehudhuria kikao kazi hicho cha siku mbili.



*Baadhi ya washiriki wakifuatilia mada wakati wa kikao kazi baina ya WCF na maafisa kazi kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania bara*

# WCF yaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu fidia kwa wafanyakazi

**Na Mwandishi wetu**

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umeendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya fidia kwa wafanyakazi wanaoumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi pamoja na masuala ya msingi ya kulinda usalama na afya mahali pa kazi.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma Septemba 17, 2024 mjini Iringa wakati akifungua kikao kazi kilichoandaliwa na mfuko huo kwa Maafisa Tawala, Maafisa Utumishi na Maafisa Usalama na Afya mahali pa kazi kutoka mikoa ya Iringa na Njombe, Songwe, Dodoma, Arusha na Dar es Salaam.

Naye Mkurugenzi wa Huduma za Tathmini WCF Dkt. Abdulsalaam Omar alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo washiriki kuhusu namna ya kutoa taarifa kwa wakati kuhusu ajali na magonjwa yanayotokana na kazi, vilevile namna ya kubaini viashiria vya hatari katika sehemu za kazi.

"Pia mafunzo haya yatawezesha washiriki kuwasaidia wafanyakazi wenzao katika maeneo yao ya kazi kukuza mbinu za kudhibiti ajali na magonjwa yatokanayo na kazi" asema Dkt. Omar.

Kwa upande wake mmoja wa washiriki wa mafunzo kutoka Benki ya Biashara (TCB) Bw. Wiliam Mwakila amesema mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yamewapa washiriki maarifa ambayo yatasaidia kubaini vihatarishi maeneo ya kazi kwa wepesi na pia wameelewa taratibu za kufuata ili kutoa taarifa na kulipwa fidia pale mtumishi anapopata changamoto ya ajali kazini.

Katika kikao kazi hicho mada mbalimbali ziliwasilishwa ikiwa ni pamoja na taratibu za uwasilishaji madai kwa njia ya mtandao, haki na wajibu wa mwajiri na mwajiriwa katika kuwezesha WCF kushughulikia kwa -



*Baadhi ya Washiriki wa Kikao kazi hicho katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa WCF Dkt. John Mduma*

Dkt. Mduma alisema pamoja na jukumu la msingi la kutoa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kuugua kutokana na kazi, kulipa wategemezi wa mfanyakazi atakayefariki kutokana na kazi, kukusanya michango pia WCF ina jukumu la kukuza mbinu za kuzuia ajali, magonjwa ama vifo katika maeneo ya kazi.

"Ni matumaini yangu kuwa kupitia kikao kazi hiki mafunzo yatakayotolewa yatasaidia kujenga uelewa kwa washiriki kuhusu shughuli za WCF, wajibu wa waajiri na waajiriwa kuhusu fidia kwa wafanyakazi pamoja na kulinda na kudumisha usalama na afya mahali pa kazi, ikiwemo udhibiti vihatarishi," alieleza Dkt. Mduma

ufanisi madai ya fidia kwa wafanyakazi na kanuni muhimu za kuzingatia ili kulinda na kudumisha usalama na afya mahali pa kazi.




*Meneja Tathmini ya Vihatarishi Mahala pa Kazi wa WCF Bi. Naanjela Msangi akiwasilisha mada katika kikao kazi hicho*

# Waziri Kikwete: Malezi bora kwa watoto ndio ustawi wa vijana wa baadae




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete akikabidhi vyerehani 30 vya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya watoto wanaolelewa katika Makao ya Taifa ya Kulelea Watoto Kikombo, Jijini Dodoma.*

## Na Mwandishi wetu

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete amesema Serikali imeweka mipango na mikakati ya kuhakikisha watoto wanapata malezi bora yanayolenga kukuza ustawi wao.

Mhe. Ridhiwani amebainisha hayo mwezi Agosti, 2024 wakati akikabidhi vyerehani 30 vya mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya watoto wanaolelewa katika Makao ya Taifa ya Kulelea Watoto Kikombo, Jijini Dodoma. Msaada wa vyerehani hivyo ulitolewa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Alisema dhamira ya serikali inayoongozwa na Mhe. Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuboresha ustawi na malezi ya watoto nchini ambao ni vijana na wataalamu wa baadae na kutoa wito kwa wizara, walezi na idara zinazohusika kuwashirikisha wadau wa maendeleo ya jamii ili kuhakikisha vituo vya kulelea watoto vinafanana katika utoaji wa huduma bora.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Bi. Zuhura Yunus alisema ugawaji wa vyerehani hivyo ni hatua nzuri kwa WCF kutambua umuhimu wa kundi hilo la watoto kupata ujuzi na maarifa kama walivyo watoto wengine.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma alisema vyerehani ambavyo vimekabidhiwa katika kituo hicho ni utekelezaji wa sera ya Mfuko ya kurejesha kwa jamii na miongoni mwa walengwa wakuu ni pamoja na makundi maalum katika jamii wakiwemo watoto.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Ridhiwani Kikwete akikabidhi matunda kwa watoto-kikombo, jijini Dodoma*

# Serikali kupitia WCF itaendelea kulinda nguvu kazi

**Na Mwandishi wetu**



*Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Patrobas Katambi akizungumza Mjini Morogoro, wakati wa mafunzo ya tathmini kwa Madaktari.*

Serikali kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakaz (WCF) itaendelea kulinda nguvu kazi ya Taifa kwa wivu mkubwa.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Patrobas Katambi, wakati akifungua mafunzo ya tathmini za ulemavu na magonjwa yatokanayo na kazi, kwa madaktari kutoka Kanda ya Mashariki na Kusini yaliyoandaliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Mwezi Agosti, Mjini Morogoro.

Alisema kwamba WCF ipo kwa ajili ya kulinda na kuhakikisha kuwa wafanyakazi wanaopata ajali kazini ama magonjwa yatokanayo na kazi wanapata fidia stahiki na ikiwa watafariki kwa ajali au magonjwa yatokanayo na kazi basi familia zao zinanufaika na fidia.

"Mtaona jinsi Serikali ilivyo na mpango mzuri wa kuhakikisha watu wake au nguvu kazi ya taifa inalindwa kwa wivu mkubwa, tunalinda mitaji ya wawekezaji, tunalinda hali za mfanyakazi, lakini pia familia zao. Mtu anaweza kupata madhila ya ulemavu wa kudumu lakini ili kuhakikisha haingii kwenye umasikini, ndio maana kuna chombo cha WCF chenye jukumu la kutoa mafao." alisisitiza

Alisema ili kuhakikisha jambo hilo linatekelezwa kwa ufanisi, WCF imekuwa ikiimarisha mifumo yake ya kutekeleza jukumu hilo ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa madaktari ambao ndio wanahusika kutibu na kufanya tathmini.


*Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) Dkt. John Mduma akizungumza Mjini Morogoro, wakati wa mafunzo ya tathmini kwa Madaktari.*

Alisema kwamba hadi kufikia Mwezi Agosti 2024, mafunzo ya tahmini za ulemavu yamewafikia madaktari zaidi ya 1,508 nchi nzima, huku madaktari wengine 84 wakinufaikana mafunzo ya kibobezi katika kufanya tathmini.


*Baadhi ya washiriki wakifuatilia mafunzo*

Naye Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dkt. John Mduma alisema madhumuni ya mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo madaktari kutoka hospitali za serikali na binafsi nchini, kuhusu namna ya kufanya tathmini ya ulemavu na magonjwa yanayotokana na kazi "Uelimishaji huu ni mkakati wa WCF kuhakikisha kwamba kila kona ya Tanzania kunakuwa na daktari mwenye ujuzi wa kufanya tathmini za ulemavu na magonjwa yanayotokana na kazi." Alifafanua.

Akieleza zaidi kuhusu mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Huduma za Tathmni, WCF, Dkt. Abdulsalaam Omar alisema kuwa mafunzo hayo yamehusisha makundi mawili, kundi la kwanza ni la madaktari waliopatiwa mafunzo ya msingi ya kufanya tathmini za ulemavu na magonjwa yatokanayo na kazi, pamoja na sheria ya fidia kwa wafanyakazi kwa maana ya utekelezaji wa shughuli za Mfuko kwa ujumla na kundi la pili ni ambao tayari walishapatiwa mafunzo ya msingi ya kufanya tathmini za ulemavu na magonjwa yatokanayo na kazi ambapo kwa awamu hiyo walipatiwa mafunzo ya vitendo zaidi.

Naye Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Mapafu, kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dkt. Paulina Chale alisema mafunzo hayo yamemjengea uelewa na uwezo katika kufanya tathmnini kwa magonjwa wanaofika ambao wengi wao wanatokea migodini.

# Picha za Matukio Mbalimbali



*Aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa iliyokuwa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kuanzia 2021 hadi Julai 2024*

























# Joke Corner



WCF
Workers Compensation Fund

# WCF ONLINE SELF SERVICE PORTAL

## https://portal.wcf.go.tz

## Pata Huduma za WCF Mtandaoni

1. Online employers' registration & issuance of eletronic certificate (Usajili wa waajiri na hati ya usajili)
2. Online payment of contribution through generation of control numbers & issuance of electronic receipts (Kuwasilisha michango ya kila mwezi kupitia namba ya udhibiti na kupata stakabadhi)
3. online changes of employees' and employers' particulars (Kuhuisha taarifa za wafanyakazi na mwajiri)
4. Online submission of return of annual earnings (Kuwasilisha Taarifa ya Mapatoya Mwaka ya Wafanyakazi)
5. Online submission of notification for occupational accidents, diseases and deaths (Kuwasilisha taarifa ya ajali, ugonjwa ama kifo kitokanacho na kazi)
6. Online claims tracking (Kupata mrejesho wa madai ya fidia)

*"Adequate and Equitable Compensation"*

www.wcf.go.tz info@wcf.go.tz 0800 11 00 28

**Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)**

Jengo la Kambarage,
Ghorofa ya 3,
S. L. P 329, 41104 Dodoma.

info@wcf.go.tz www.wcf.go.tz 0800 11 00 28